**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**

KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA USTAWI NA MAENDELEO YA JAMII

# TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA USTAWI NA MAENDELEO YA JAMII KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUMU KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA OFISI HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027

**----------------**

*[Imetolewa kwa mujibu wa Kanuni 121 (5) ya Kanuni za*

*Kudumu za Bunge, Toleo la, 2025]*

Idara ya Kamati za Bunge,
Ofisi ya Bunge,
10 Barabara ya Morogoro,
S. L. P. 941,
40490 Tambukareli,
**DODOMA.**

**1 Juni 2026**

# YALIYOMO

**YALIYOMO** ........ **i**
**ORODHA YA VIELELEZO** ........ ii
**SEHEMU YA KWANZA** ........ **1**
**1.0 MAELEZO YA JUMLA** ........ **1**
1.1 Utangulizi ........ 1
1.2 Msingi wa Uchambuzi ........ 2
1.3 Mawanda ya Uchambuzi wa Taarifa ........ 3
**SEHEMU YA PILI** ........ 5
2.1 Uzingatiaji wa Ushauri wa Kamati ........ 6
2.2 Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa Fedha ........ 8
2.2.1 Ufafanuzi wa Jumla ........ 8
2.2.2 Yatokanayo na Ukaguzi wa Miradi ........ 10
2.3 Utekelezaji wa Vipaumbele na Majukumu ya Wizara. ........ 11
2.3.1 Hatua iliyofikiwa katika Ukusanyaji wa Maduhuli ........ 13
2.3.2 Hatua iliyofikiwa katika ukusanyaji wa Maduhuli ........ 13
2.3.3 Mwenendo wa Upatikanaji wa fedha kutoka Hazina ........ 14
**SEHEMU YA TATU** ........ 16
**3.0 UCHAMBUZI WA MPANGO NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027** ........ 16
3.1 Makadirio ya Mapato ........ 16
**SEHEMU YA NNE** ........ 19
**4.0 MAONI NA USHAURI** ........ 19
4.1 Maoni ya Jumla ........ 19
4.2 Ushauri wa Kamati ........ 19
4.2.1 Ukusanyaji wa Maduhuli ........ 19
4.2.2 Upatikanaji wa Fedha ........ 20
4.2.3 Sekta ya Maendeleo ya Jamii ........ 20
4.2.4 Utoaji wa Mikopo ........ 21
4.2.5 Sekta ya Ustawi wa Jamii ........ 21
**SEHEMU YA TAN0** ........ 24
**5.0 HITIMISHO** ........ 24

# ORODHA YA VIELELEZO

**Kielelezo Na. 1:** Upatikanaji wa Fedha kwa Fungu 53 ...................................... 15

**Kielelezo Na. 2:** Mchanganuo wa Makadirio ya Maduhuli ............................. 17

**Kielelezo Na. 3:** Ulinganisho wa Makadirio ya Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 na Mwaka 2026/2027 - Fungu 53 .............. 18

**TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA USTAWI NA MAENDELEO YA JAMII KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUMU KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027**

## SEHEMU YA KWANZA

## 1.0 MAELEZO YA JUMLA

### 1.1 Utangulizi

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa **Kanuni ya 121 (5)** ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2025, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii Kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 pamoja na Maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

**Mheshimiwa Spika**, ili kurahisisha mtiririko wa maudhui pamoja na kuzingatia masharti ya Kanuni ya 145 ya Kanuni za Bunge,inayohusu taarifa yoyote ya Kamati inayowasilishwa Bungeni, taarifa hii imegawanyika katika sehemu kuu tano (05) kama ifuatavyo: -

i) Sehemu ya Kwanza inahusu Msingi na Mawanda ya Uchambuzi;
ii) Sehemu ya Pili inahusu uchambuzi na tathmini ya utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii,Jinsia,Wanawake na Makundi Maalum;
iii) Sehemu ya Tatu inahusu uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2026/2027;
iv) Sehemu ya nne inafafanua maoni na ushauri wa Kamati unaotolewa kwa Serikali; na
v) Sehemu ya Tano inahitimisha taarifa ya uchambuzi na kuonesha msimamo wa Kamati.

## 1.2 Msingi wa Uchambuzi

**Mheshimiwa Spika**, msingi wa Kamati wa kuchambua Taarifa ya Utekelezaji wa Majukumu na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum unawekwa na Masharti ya Kanuni za Bunge, Kifungu cha 6 (5)(b) kikisomwa kwa pamoja na Kifungu cha 7 (1)(a) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge, vinaipa Kamati jukumu la kufanya uchambuzi wa Bajeti na Makadirio ya Wizara hii.

Aidha, kwa mujibu wa Kanuni ya 120(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge imeweka masharti yanayotaka Taarifa ya

Utekelezaji na Makadirio ya Wizara hii kuchambuliwa na Kamati kabla ya kujadiliwa Bungeni.

**Mheshimiwa Spika**,ili kukidhi masharti hayo, Kamati ilipokea na kujadili Taarifa ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii,Jinsia,Wanawake na Makundi Maalum kuhusu Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa Fedha 2026/2027. Katika hatua hiyo,Kamati ilifanya uchambuzi wa kina na kuja na matokeo kama yalivyoainishwa katika taarifa hii.

### 1.3 Mawanda ya Uchambuzi wa Taarifa

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa ya Kamati inahusu Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum **(Fungu 53)** kwa mwaka wa fedha 2025/2026 pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2026/2027.

**Mheshimiwa Spika,**uchambuzi uliofanyika uligusa maeneo yafuatayo:-

i) Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii,Jinsia,Wanawake na Makundi Maalum kwa mwaka wa Fedha 2025/2026;

ii) Makadirio ya Mapato kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027;na

iii) Makadirio ya Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027;na

**Mheshimiwa Spika,** wakati wa uchambuzi, Kamati iliongozwa na kigezo cha asilimia pamoja na kufanya tathmini ya jumla na ulinganisho wa mambo mbalimbali. Mambo hayo yaliiwezesha Kamati kubaini hatua iliyofikiwa katika utekelezaji na mantiki ya mpango na makadirio kwa mwaka wa fedha unaokuja.

## SEHEMU YA PILI

## 2.0 UCHAMBUZI WA UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026

**Mheshimiwa Spika,** sehemu hii ya taarifa inaripoti matokeo ya utekelezaji wa masharti ya Kanuni ya 120 (2) ya Kanuni za Bunge. Kanuni hiyo inazitaka Kamati za Bunge za Kisekta kuchambua taarifa za utekelezaji wa Bajeti za Wizara inazozisimamia kwa mwaka wa fedha unaoisha na kufanya ulinganisho wa makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha unaofuata.

**Mheshimiwa Spika,** ili kukidhi masharti hayo tarehe 24 Machi,2026, Kamati ilipokea taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2025/2026 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2026/2027. Taarifa hiyo ilijumuisha Mpango na Bajeti ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii,Jinsia,Wanawake na Makundi Maalum kwa **Fungu 53.**

**Mheshimiwa Spika,** baada ya hatua hiyo,Kamati inatoa taarifa kuhusu mambo yafuatayo:-

i) Uzingatiaji wa Maoni na Ushauri wa Kamati;
ii) Ukaguzi wa Miradi;
iii) Utekelezaji wa Vipaumbele;
iv) Hali ya Ukusanyaji wa Maduhuli;na

v) Hali ya upatikanaji wa Fedha

**Mheshimiwa Spika,** mambo hayo kwa pamoja yanaweka msingi wa kuliwezesha Bunge lako Tukufu kupata uwiano utakaolisaidia katika kufikia uamuzi baada ya mjadala wa hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Wizara ya Maendeleo ya Jamii,Jinsia,Wanawake na Maakundi Maalum kama ilivyowasilishwa na Mtoa hoja.

## 2.1 Uzingatiaji wa Ushauri wa Kamati

**Mheshimiwa Spika**, katika kulisaidia Bunge kutekeleza jukumu lake la kuishauri Serikali tarehe 27 Mei,2025 wakati wa uwasilishaji wa hotuba ya Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum kwa mwaka fedha 2025/2026, Kamati ilitoa Maoni na Ushauri kuhusu mambo kumi na moja (11) kwa Fungu 53.

Naomba kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa baadhi ya maeneo ushauri wa kamati umezingatiwa huku maeneo mengine utekelezaji wa ushauri wa Kamati haujafanyiwa kazi kwa kiwango cha kuridhisha.

**Mheshimiwa Spika,**Mfano wa ushauri uliozingatiwa ni wa kutoa fedha kwa ajili ya mikopo nafuu kwa wafanya biashara ndogondogo ambapo wafanyabiashara **6306**

wamenufaika na mikopo hiyo yenye thamani ya **Shilingi Bilioni 13,156,183,022/=**

**Mheshimiwa Spika,**hata hivyo,Kamati ilibaini kuwa kuna baadhi ya maoni na ushauri ambao utekelezaji wake hauridhishi kama ifuatavyo:-

i) Kuandaa mkakati maalum unaotekelezeka wa kupima na kupata Hati za maeneo yote ya Vyuo na Vituo ambavyo havijapimwa;
ii) Kuendeleza maeneo makubwa yanayomilikiwa na Taasisi,Vyuo na vituo vilivyo chini ya Wizara kwa shughuli mbalimbali za kiuchumi;
iii) Kuweka mikakati Madhubuti ya ufuatiliaji na uhamasishaji wa mashirika yasiyo ya kiserikali kulipa ada ili kuongeza mapato ya Serikali;na
iv) Kuandaa mkakati wa kutoa elimu juu ya faida za kujisajili na manufaa yatokanayo na usajili wa Wafanyabiashara ndogondogo.

**Mheshimiwa Spika**, hata hivyo,Kamati ilibaini kuwa ukomo wa bajeti na upatikanaji usioridhisha wa fedha za Maendeleo ni moja ya sababu za Wizara kushindwa kutekeleza baadhi ya maoni na ushauri wa kamati kwa ufanisi. Hali hii inaweza kupunguza manufaa ya Wizara hii katika Taifa na kupelekea kuzorotesha ustawi wa wananchi hapa Nchini.

## 2.2 Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa Fedha

### 2.2.1 Ufafanuzi wa Jumla

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 120 (1) ya Kanuni za Bunge,Kamati ilifanya ziara katika Mikoa mitatu (03) Arusha, Kilimanjaro, na Dar es Salaam. Katika mikoa hiyo Kamati ilikagua miradi mitatu ambayo ni sehemu ya miradi iliyotengewa fedha kiasi cha **Shilingi 26,941456,000** kwa mwaka wa fedha 2025/2026.Naomba kubainisha na kufafanua miradi hiyo pamoja na kufanya majumuisho ya mambo yaliyojitokeza katika ukaguzi wa miradi kama ifuatavyo:-

**(A) Mradi 6330: Ujenzi wa Jengo la Utawala katika Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru.**

**Mheshimiwa Spika**, mradi huu upo katika mwendelezo wa utekelezaji ambapo katika mwaka wa fedha 2025/2026 ulipokea **Shilingi 600,000,000** ambapo mpaka Kamati inatembelea eneo la mradi **shilingi 1,200,000,000** zilikuwa zimetolewa kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huu, na kufanya jumla ya fedha zilizopokelewa tangu kuanza kwa mradi kuwa ni **shilingi 3,900,000,000**. Jengo hilo linaundwa na kumbi za mikutano na ofisi za watumishi.

**Mheshimiwa Spika,** taarifa zilizowasilishwa mbele ya kamati zilibainisha kuwa mradi huu unapaswa kukamilika mwezi Mei Mwaka 2026 na umefika **asilimia 80** .

**(B) Mradi 6330: Utekelezaji wa mradi wa Ujenzi wa Ukumbi wa mihadhara katika Taasisi ya Ustawi wa Jamii Kijitonyama.**

**Mheshimiwa Spika,** mradi huu unatekelezwa kwa mfumo wa *force accaunt wenye* thamani ya **Shilingi 626,405,367.66** ambapo hadi Kamati inatembelea ilikuwa imetumia kiasi cha **Shilingi 394,741,341.65** na mradi umefikia **asilimia 82** na utakuwa na uwezo wa kubeba Wanafunzi 400 kwa wakati mmoja

**(C) Mradi 6279: Ukarabati wa makazi ya wazee.**

**Mheshimiwa Spika,** mradi huu kamati ilitaka kujionea tija inayoweza kupatikana iwapo makazi ya Wazee yataboreshwa kwa kuzingatia vigezo mbalimbali, ili kufanikisha hilo Kamati ilifanya ziara katika makazi ya Wazee Njoro ambayo kwa kiasi kikubwa yamekarabatiwa na wadau wa maendeleo. Katika ziara hii Kamati ilipata fursa ya kujionea kuwa ipo haja ya serikali kuona namna

ya kuongeza Bajeti ili kuweka kwenye mpango makazi mengi zaidi tofauti na hali ya hivi sasa ambapo makazi machache huwekwa kutokana na ufinyu wa Bajeti, aidha Kamati imebaini changamoto mbalimbali kwenye makazi haya zinazohitaji msukumo wa kibajeti. Mathalani, katika mwaka wa fedha 2025/2026 Wizara ilitengewa kiasi cha **shilingi 1,000,000,000** ambapo hadi Kamati ilipotembelea mradi **shilingi 568,000,000** zilikuwa zimepokelewa ikiwa ni robo ya tatu ya utekelezaji wa bajeti

### 2.2.2 Yatokanayo na Ukaguzi wa Miradi

**Mheshimiwa Spika,** katika ziara za ukaguzi wa miradi inayotekelezwa na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia,Wanawake na Makundi Maalum, Kamati ilipokea taarifa za utekelezaji wa miradi na kuona hali halisi kwenye maeneo ya utekelezaji wa miradi husika. Lengo ilikuwa kulinganisha na kubaini iwapo taarifa zilizowasilishwa na Wizara zinawiana na hatua zilizofikiwa katika utekelezaji pamoja na madhumuni ya miradi inayohusika

**Mheshimiwa Spika,**Tathmini ya Kamati imebainisha kuwa:-

i) Utekelezaji wa sehemu kubwa ya miradi iliyotembelewa na kukaguliwa na kamati imezingatia thamani ya fedha na hatua iliyofikiwa

inawiana na muda wa utekelezaji wa miradi husika;

ii) Miradi iliyotembelewa na Kamati ingekuwa na tija kubwa zaidi na ufanisi kama fedha za maendeleo zingetolewa kwa wakati kama ilivyokusudiwa; na

iii) Sehemu kubwa ya miradi iliyotembelewa inatumia Force Account jambo linalopongezwa na kamati na litakalochochea utekelezaji wenye tija.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Serikali kwa hatua mbailmbali zilizofikiwa katika utekelezaji wa miradi chini ya Wizara ya Maendeleo ya jamii,Jinsia,Wanawake na Makundi Maalum (**Fungu 53**) .Kamati inalitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa katika kutekeleza miradi hiyo thamani ya fedha, uwekezaji, ufanisi na tija vimezingatiwa.

## 2.3 Utekelezaji wa Vipaumbele na Majukumu ya Wizara.

**Mheshimiwa Spika,** tarehe 24 Machi,2026 kamati ilipokea na kuchambua taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum **(Fungu 53)** kwa mwaka wa fedha 2025/2026, wakati wa uchambuzi wake Kamati ilizingatia vipaumbele vya wizara ambavyo ni:-

i) Kukuza ari ya jamii kushiriki katika kupanga na kutekeleza Sera na Miradi ya Maendeleo iliyoibuliwa Ngazi ya Msingi;
ii) Kuratibu afua za Upatikanaji wa Haki, Ulinzi, Malezi na Matunzo ya watoto;
iii) Kuratibu afua za kukuza usawa wa kijinsia,kutokomeza ukatili wa kijinsia na uwezeshaji wa wanawake kiuchumi;
iv) Kuratibu na kuimarisha utoaji wa huduma za ustawi wa jamii;
v) Utambuzi,uratibu na uendelezaji wafanyabiashara Ndogondogo

**Mheshimiwa Spika,**Wizara imefanikiwa kufanya baadhi ya shughuli ili kutekeleza vipaumbele ilivyojiwekea, baadhi ya shughuli hizo ni pamoja na:-

i) mapitio ya Mwongozo wa majukumu ya wataalam wa maendeleo ya jamii wa Mwaka 2018,Toleo la Mwaka 2025;
ii) uanzishwaji wa Madawati ya ulinzi na usalama wa Mtoto;
iii) Imetoa mafunzo ya kujenga uelewa kuhusu programu ya kizazi chenye usawa;na
iv) Wizara kwa kushirikiana na OWM- TAMISEMI imeweza kuwapatia vitambulisho vya kidigitali kwa wafanyabiashara ndogondogo kwa ajili ya

kuvitumia kuomba mkopo yenye masharti mafuu kutoka Taasisi za kifedha.

### 2.3.1 Hatua iliyofikiwa katika Ukusanyaji wa Maduhuli

**Mheshimiwa Spika**, lengo la uchambuzi wa taarifa za makusanyo ya maduhuli ni kuliwezesha Bunge kubaini iwapo lengo la makusanyo lililoidhinishwa na Bunge limefanikiwa.Aidha,uchambuzi huu unaliweka Bunge katika nafasi ya kutumia uzoefu unaopatikana kwa mwaka wa fedha 2025/2026 na kubaini uhalisia inavyostahili kwa mwaka wa fedha 2026/2027.Kamati ilifanya uchambuzi kwa kuzingatia masuala yafuatayo:-

i) Kiasi kilichokusanywa ikilinganishwa na lengo la makusanyo;na
ii) Ulinganisho wa kipindi kama hicho kwa mwaka wa fedha 2024/2025.

### 2.3.2 Hatua iliyofikiwa katika ukusanyaji wa Maduhuli

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2025/2026, Wizara ya Maendeleo ya Jamii,Jinsia,Wanawake na Makundi Maalum **Fungu 53** ilikadiriwa kukusanya jumla ya **Shilingi 9,040,129,000/=**

Hadi kufikia Februari,2026 wizara ilikuwa imekusanya **Shilingi 2,991,829,587/=** sawa na **asilimia 33.09 tu** ya lengo la

makusanyo ukilinganisha na muda wa utekelezaji wa bajeti ambao ni **asilimia 66.7**

**Mheshimiwa Spika**, Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa uwezekano wa Wizara kufikia lengo la ukusanyaji ni mdogo kwani katika kipindi cha miaka mitatu mfulululizo makusanyo ya Wizara yamekuwa chini ya **asilimia 50** ya lengo la makusanyo lililoidhinishwa na Bunge.

### 2.3.3 Mwenendo wa Upatikanaji wa fedha kutoka Hazina

**Mheshimiwa Spika,** utekelezaji wa Bajeti unategemea mwenendo wa upatikanaji wa fedha kutoka hazina kama zilivyoidhinishwa na Bunge. Kamati ilipokea na kuchambua mwenendo wa upatikanaji wa fedha kwa Fungu 53 kutoka hazina kama ifuatavyo:-

i) Upatikanaji wa jumla ya Fedha zilizoidhinishwa kwa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum **Fungu 53** ni **asilimia 67.8** ya bajeti ikiwa ndani ya utekelezaji wa kipindi kama hicho;
ii) Fedha za matumizi ya kawaida zilizopatikana kwa **asilimia 66 ;**
iii) Fedha za Matumizi mengineyo (OC) zimepokelewa kwa **asilimia 67 ;**

iv) Fedha za mishahara zilizopokelewa ilikuwa **asilimia 65** ikiwa na upungufu wa **asilimia 1.7** ya fedha iliyotakiwa katika kipindi kama hiki;

v) Fedha za kugharamia utekelezaji wa miradi ya maendeleo zilipatikana kwa **asilimia 70** ya Bajeti; na

vi) Katika fedha za kugharamia miradi ya maendeleo,Fedha za Ndani zilifikia **asilimia 87** na Fedha za nje **asilimia 48.**

Upatikanaji wa fedha kutoka hazina kwa ajili ya miradi ya maendeleo ni wa kuridhisha na hivyo Kamati inaishauri Serikali kusimamia miradi kikamilifu ili ilete tija iliyokusudiwa kwa Wananchi.

**Kielelezo Na. 1: Upatikanaji wa Fedha kwa Fungu 53**

| AINA YA MATUMIZI | BAJETI ILIYOIDHINISHWA | KIASI KILICHOPOKELEWA | ASILIMIA |
|---|---|---|---|
| Mshahara | 22,646,148,000 | 14,797,974,939 | 65 |
| Matumizi mengineyo | 26,469,549,000 | 17,799,823,321 | 67 |
| Jumla Ndogo | 49,115,697,000 | 32,597,798,260 | 66 |
| Miradi ya Maendeleo | 26,941,456,000 | 18,948,732,400 | 70 |
| **Jumla kuu** | **76,057,153,000** | **51,546,530,666** | **67.8** |

**Chanzo:** Randama za Wizara, 2026 na Usanifu wa Kamati

## SEHEMU YA TATU

## 3.0 UCHAMBUZI WA MPANGO NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027

**Mheshimiwa Spika,**Kamati ilichambua na kujadili Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii,Jinsia Wanawake na Makundi Maalum kwa mwaka wa fedha 2026/2027.

Uchambuzi wa Kamati ulijielekeza katika maeneo yafuatayo:-

i) Makadirio ya Mapato kwa mwaka wa fedha 2026/2027;na
ii) Makadirio ya Matumizi kwa mwaka wa fedha 2026/2027.

### 3.1 Makadirio ya Mapato

**Mheshimiwa Spika**, kwa kutambua uhusiano uliopo kati ya Mapato na matumizi, kamati ilipokea ufafanuzi kuhusu lengo la maduhuli kwa mwaka wa fedha 2026/2027 ambapo Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum **(Fungu 53)** inakadiriwa kukusanya maduhuli ya Shilingi **7,040,129,000/=**. Uchambuzi wa kamati umebaini kuwa makusanyo yamepungua kwa **Shilingi 2,000,000,000** sawa **na asilimia 22.1** ikilinganishwa na makadirio ya makuasanyo kwa mwaka wa Fedha

2025/2026. Pamoja na kupunguziwa maduhuli kamati ilipewa taarifa kuwa Wizara iliibua chanzo kipya cha mapato cha ulipaji wa kodi kwa shule za Watoto za kulala mchana (daycare centers) na kwa lengo la kuongeza uwajibakaji na heshima katika kutoa huduma.

**Kielelezo Na. 2: Mchanganuo wa Makadirio ya Maduhuli**

| FUNGU | Mwaka 2025/2026 | Mwaka 2026/2027 | Ongezeko/ pungufu | Asilimia |
|---|---|---|---|---|
| Wizara (53) | 9,040,129,000 | 7,040,129,000 | 2,000,000,000 | 22.1 |

**Chanzo:** Randama za Wizara, 2026 na Usanifu wa Kamati

### 3.2 Makadirio ya Matumizi

**Mheshimiwa Spika**,kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 120 (2) ya Kanuni za Bunge yamelenga kuliwezesha Bunge kutumia uzoefu wa utekelezaji wa Bajeti kwa mwaka wa fedha unaoisha ili kuchambua makadirio ya matumizi kwa mwaka wa fedha unaofuata kwa kuzingatia lengo hilo, Kamati imechambua, makadirio ya matumizi kwa mwaka wa fedha 2026/2027.

**Mheshimiwa Spika,**Wizara (Fungu 53) inakadiriwa kutumia jumla ya **Shilingi 108,024,243,000/=** kwa ajili utekelezaji wa shughuli na vipaumbele vya Wizara hii. Matokeo ya uchambuzi yanaonesha kuwa:-

i) Jumla ya bajeti ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii,Jinsia,Wanawake na Makundi Maalum (**Fungu 53)** kwa mwaka wa fedha 2026/2027 imeongezeka kwa **asilimia 42.03** ikilinganishwa na mwaka wa fedha 2025/2026 hii imetokana na kuongezeka kwa fedha za miradi ya maendeleo;

ii) Bajeti ya matumizi ya kawaida kwa mwaka wa fedha 2026/2027 ni **50,137,801,000/=** sawa na **asilimia 46.4** ya Bajeti yote ya Wizara hii. Bajeti hii imeongeka kwa **asilimia 2.08** ikilinganishwa na mwaka wa fedha 2025/2026 hili ongezeko limetokana na kupatikana kwa kibali cha kuajiri Watumishi; na

iii) Bajeti ya Maendeleo kwa mwaka wa fedha 2026/2027 ni Shilingi **57,886,442,000/=** sawa na asilimia **53.6** ya bajeti yote. Hata hivyo, bajeti hii imeongezeka kwa **asilimia 114.86** ikilinganishwa na mwaka wa fedha 2025/2026

**Kielelezo Na. 3: Ulinganisho wa Makadirio ya Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 na Mwaka 2026/2027 - Fungu 53**

| AINA YA MATUMIZI | MWAKA 2025/2026 | MWAKA 2026/2027 | ASILIMIA Ongezeko/ Upungufu |
|---|---|---|---|
| Mishahara | 22,646,148,000 | 23,315,207,000 | 2.95 |
| Matumizi mengineyo | 26,469,549,000 | 26,822,594,000 | 1.33 |
| Jumla | 49,115,697,000 | 50,137,801,000 | 2.084 |
| Miradi ya Maendeleo | 26,941,456,000 | 57,886,442,000 | 114.86 |
| **Jumla kuu** | **76,057,153,000** | **108,024,243,000** | **42.03** |

## SEHEMU YA NNE

# 4.0 MAONI NA USHAURI

## 4.1 Maoni ya Jumla

i) Wizara iendelee kutoa elimu kwa wanawake inayolenga kuwaonesha ni kwa namna gani wanaweza kunufaika na fursa mbalimbali zinazoweza kupatikana katika mchakato wa utekelezaji wa Bajeti ya Serikali; na

ii) Wizara iendelee kutoa elimu kwa jamii juu ya umuhimu na misingi bora ya malezi na makuzi ya mtoto;

## 4.2 Ushauri wa Kamati

### 4.2.1 Ukusanyaji wa Maduhuli

Kamati inashauri Serikali kuwa:-

i) iongeze kasi ya ukusanyaji wa maduhuli ya Serikali kupitia uuzaji wa mitaala ya vyuo vya maendeleo ya jamii na ada ya malazi kwa wanafunzi wa vyuo vya Maendeleo ya jamii kwani imekuwa na mwenendo usioridhisha katika ukusanyaji;

ii) iendelee kuibua vyanzo vipya vya ukuanyaji wa maduhuli ya Serikali;na

iii) iweke mikakati madhubuti ya uhamasishaji na ufuatiliaji wa ulipaji wa ada za Mashirikia yasiyo ya Kiserikali.

#### 4.2.2 Upatikanaji wa Fedha

Kamati inaishauri Serikali kuwa:-

i) itoe fedha za miradi ya Maendeleo kama ilivyoidhinishwa na Bunge lako Tukufu ili kuweza kutekeleza shughuli kama zilivyopangwa; na

ii) iongeze bajeti kwa ajili ya kutekeleza majukumu na vipaumbele kama ilivyopangwa ;

#### 4.2.3 Sekta ya Maendeleo ya Jamii

Kamati inaishauri Serikali kuwa

i) iweke mikakati na jitihada za kubadili mitaala ya vyuo kwa lengo la kuzalisha Maafisa maendeleo ya jamii watakaoendana na kasi ya maendeleo iliyopo;

ii) itengeneze vituo atamizi (incubation centres) vingi kwa shughuli mbalimbali ili kuwezesha makundi maalum kupata elimu za ujasiliamali,ujuzi,masuala ya fedha na biashara ili iweze kuwasaidia kuwa na shughuli endelevu pindi wanapopewa mikopo;

iii) iongeze kasi ya kuhuisha sera ya maendeleo ya jamii ya mwaka 1996 ili iendane na wakati uliopo kwa lengo la kurahisisha mchakato wa kutunga Sheria ya Maendeleo ya Jamii; na

iv) ianzishe bodi ya utaalamu (professinal board) za maendeleo ya jamii kwa ajili ya kupata wataalam wabobezi na watakaoendana na soko la ajira lililopo;

### 4.2.4 Utoaji wa Mikopo ya Wafanyabiashara Ndogondogo

Kamati inaishauri Serikali kuwa:-

i) iendelee kutoa elimu kwa Wafanyabiashara ndogondogo juu ya kujiandikisha katika Mfumo wa Utambuzi na Usajili wa Wafanyabiashara Ndogondogo ;

ii) iongeze kasi katika utoaji wa mikopo kwa wafanyabiashara ndogondogo ili kuongeza idadi ya wanufaika wa fursa hiyo inayotolewa na Serikali; na

iii) iongeze kasi ya kufuatilia marejesho ya mikopo ya Wafanyabiashara ndogondogo ili kutoa fursa kwa wengi zaidi.

### 4.2.5 Sekta ya Ustawi wa Jamii

Kamati inaishauri Serikali kuwa

i) iendelee kuajiri Maafisa ustawi wa jamii ili kukidhi mahitaji yaliyopo kwasasa, jambo litakalosaidia uwepo wa wataalam hao katika maeneo muhimu kama vile hospitalini, shuleni, mahabusu, mahakamani na sehemu nyingine;

ii) ianze mchakato wa kuunda bodi ya Wataalam wa Ustawi wa jamii kwa lengo la kupata Wataalam bora na watakaoendana na soko la ajira la sasa;

iii) iongeze Fedha kwa ajili ya kutoa huduma za ustawi wa jamii nchini ikiwa ni pamoja kutoa fedha kadri zilivyoidhinishwa na Bunge;

iv) itenge fungu Maalum la Kibajeti kwa ajili ya kutoa huduma za malezi na makuzi na maendeleo ya awali kwa mtoto ;

v) Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu,Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na Sekta binafsi iongeze kasi ya ujenzi wa vituo salama vya malezi ya mtoto ili maeneo mengi nchini yaweze kufikiwa na huduma hiyo;

vi) iongeze msisitizo kwenye malezi na makuzi ya mtoto ili kuendana na mikataba ya malezi ya kimataifa;

vii) iongeze nguvu katika ufuatiliaji wa mwenendo wa utekelezaji wa takwa la kisheria la kutenga asilimia 3% ya makusanyo ya Halmashauri kwa ajili ya malezi na makuzi ya mtoto kwenye maeneo husika;

viii) iweke msisitizo katika utoaji wa elimu inayohusu afya ya akili kwa shule za awali na msingi hapa nchini ili kujenga kizazi chenye fikra chanya;

ix) itafute namna bora ya kuweza kutekeleza Sera ya matibabu bure kwa makundi maalum;

x) ihuishe Sheria ya ndoa ya mwaka 1971 kwa ajili ya kuondoa kukinzana na Sheria ya mtoto ya mwaka 2009.

## SEHEMU YA TAN0

## 5.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika**, napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha taarifa hii. Aidha, napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii ambao maoni, ushauri na ushirikiano wao umewezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi na hatimaye kukamilika kwa taarifa hii. Naomba majina yao yaingie kwenye kumbukumbu za kudumu za Bunge kama yalivyo wasilishwa katika taarifa hii; nayo ni kama ifuatavyo: -

1. Mhe.Hawa Chakoma Mchafu, Mb. – **Mwenyekiti**
2. Mhe.Dkt. Regina Christopher Malima, Mb. – **Makamu Mwenyekiti**
3. Mhe.Mohamed Abrahman Mwinyi, Mb.
4. Mhe.Mariam Nassoro Kisangi, Mb.
5. Mhe.Tinnar Andrew Chenge, Mb.
6. Mhe.Katani Ahmadi Katani, Mb.
7. Mhe.Said Ibrahim Mzimba, Mb.
8. Mhe.Lucy Similya Kombani, Mb.
9. Mhe. Nasriya Nassir Ali, Mb.
10. Mhe. Shadya Haji Omary, Mb.
11. Mhe. Mohamed Kassim Salum, Mb.
12. Mhe. Shaffin Ahmedali Sumar, Mb.

13. Mhe. Athumin Omary Mapalilo, Mb.
14. Mhe. Boniphace Mwita Getere, Mb.
15. Mhe. Pascal Lucas Lutandula, Mb.
16. Mhe. Kangi Alphaxard Lugola, Mb.
17. Mhe. Kafiti William Kafiti, Mb.
18. Mhe. Edefonce Joachim Canoni, Mb.
19. Mhe. Ahmed Ally Salum, Mb.
20. Mhe. Happiness Daniel Ngwando, Mb.

**Mheshimiwa Spika**, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati naomba nichukue fursa hii kumpongeza Mhe. Dkt. Doroth Onesphoro Gwajima, Mb, Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum na Naibu Waziri Mhe. Mha. Marryprisca Winfred Mahundi, Mb kwa kuwasilisha makadirio ya mapato na matumizi ya Ofisi yake kwa ufanisi ambapo hatua hii imeisaidia Kamati kufanya kazi yake kwa namna inayofaa.

**Mheshimiwa Spika**, naomba pia niwashukuru watendaji wote wa Wizara pamoja na taasisi zake kwa ushirikiano waliotoa kwa Kamati wakiongozwa na Katibu Mkuu Ndg. Eliakim Chacha Maswi na Manaibu Katibu Wakuu Bwn. Amon Anastaz Mpanju na Bi. Felister Mdemu.

**Mheshimiwa Spika**, mwisho lakini sio kwa umuhimu, napenda kuwashukuru Watumishi wote wa Bunge chini ya Uongozi wa Katibu wa Bunge Ndg. Baraka Ildephonce Leonard, kwa

kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake vyema na kuhakikisha shughuli zote za Kamati zinatekelezwa kikamilifu.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum (Fungu 53) kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja**.**

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja.



Hawa Chakoma Mchafu, Mb

**<u>MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA USTAWI NA MAENDELEO YA JAMII</u>**

01 Juni, 2026